## Sifa za Shule

- Kujikita katika masomo ya STEM na uongozi
- Maabara za sayansi zilizo na vifaa vya kutosha
- Maktaba na maabara ya kompyuta
- Mazingira salama na yenye utulivu
- Walimu wenye huruma na ujuzi
- Mabadilishano na ushirikiano na shule za Japani
- Fursa za kupata ufadhili wa masomo kutoka kwa wafadhili wa Japani
- Malazi na chalula kwa wanafunzi wote

## Ada za Shule

Ada za O level （Kidato cha kwanza ~ nne）ni 3,000,000Tsh/= kwa mwaka.
Ada za A level（Kidato cha tano na sita）ni 3,500,000Tsh/= kwa mwaka.
※ Gharama za sare za shule, masomo ya ziada (remedial classes), ada za mitihani, na gharama za safari za shule hazija-jumuishwa.
※ Baadhi ya wanafunzi wanafadhiliwa na kampuni na watu binafusi wa Japani.

## Namna ya Kujiunga

Shule ya wasichana Sakura inapenda kuwatangazia wazazi na walezi kuwa fomu za kujiunga na kidato cha kwanza 2026 inapatikana shuleni au kwa kupiga simu. Gharama ya fomu ni 20,000/=. Pia tuna mitihani ya kujiunga na shule itakayo-fanyika kila Jumamosi kuanzia tarehe 12 mwezi wa 9, isipokuwa tarehe26 kuanzia saa tatu asubuhi.


Wanafunzi wakiwa safari za mafunzo


Wanafunzi wakiwa katika tamaduni


Wanafunzi wakiwa shambani

## Mawasiliano


0756-596-568, 0625-984-974, 0656-685-552

https://www.sakura.vision/tz

sakura.sec.16@gmail.com


Facebook, Instagram, na YouTube zipo.

Karibuni!



# Sakura Girls Secondary School


P.O.Box 77, Bangata, Arusha, Tanznaia

## Kuhusu SGSS



Mazingira ya shule

Shule ya wasichana Sakura (Sakura Girls Secondary School, SGSS) imeanzishwa mwaka 2016 na mabibi wawili, Professor Dr. Sumiko Iwao kutoka Japani, na Bi. Frida Tomito kutoka Tanzania.

Malengo yetu ni kuwasomesha watoto wa kike wa Kitanzania kuwa viongozi wa taifa wa baadae hasa katika sekta za sayansi na teknologia. Wanafunzi wana nafasi nyingi za kutoa majadiliano na kufanya mijadala ili wajifunze jinsi ya kuwaongoza watu na kufanya ubunifu.

Pia wanafunzi wanatakiwa kuwa daraja kati ya Tanznaia na Japani. Shule inapokea msaada kutoka serikari, kampuni, na watu binafsi wa Japani. Wageni wengi wanakuja kutoka Japani na kubadilishana nao utamaduni mbalimbali na maoni tofauti.

## Miundo Mbinu

Shule iko kwenye mazingira yaliyotulia kwa kujisomea na ina madarasa, maabara na maktaba ya kisasa yenye vitabu na komputa za kutosha. Pia shule ina mabweni ya kisasa yenye vyoo na mabafu ndani, kuna ulinzi na usalama wa kutosha. Pia viwanja vya michezo vipo.

## Aina ya Shule

Shule yetu ni ya wasichana ni ya bweni tu, na inachukua wasichana wa dini zote. Vilevile shule inaendeshwa kwa kufuata taratibu zote za wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi. Tunawapokea wanafunzi kutoka kidato cha kwanza hadi kidato cha sita.

## Masomo

Masomo yanayofundishwa ni masomo ya sayansi na sanaa pia inatoa mafunzo ya masomo ya ziada kama komputa, na kujifunza utamaduni wa kijapani. Pia kuna nafasi za kuhamia kwa kidato cha kwanza, kidato cha tatu, na kidato cha tano.




Wanafunzi wakiwa maabara



Wanafunzi wakiwa darasa la Kijapani

## Maendeleo Yetu

Matokeo ya CSEE




## Habari Mpya

### -Ujenzi wa Majengo ya A Level-



Madarasa



Bweni

Mnamo Septemba 2025, jengo la madarasa kwa ajili ya elimu ya ngazi ya Advanced Level lilikamilika kujengwa kupitia mpango wa Msaada wa Ruzuku kwa Miradi ya Usalama wa Binadamu katika Ngazi ya Jamii (GGHSP) wa Serikali ya Japani. Jengo la bweni pia lilijengwa kwa msaada kutoka Group Kilimanjaro Inc., shirika letu mshirika nchini Japani.

### -Uzinduzi wa A Level-



Tangu Julai 2026, tumeanza rasmi kutoa elimu ya Advanced Level (Kidato cha tano na sita).
Sherehe ya uzinduzi wa elimu ya Advanced Level ilifanyika tarehe 25 Julai 2026, na ilihudhuriwa na Balozi wa Japani pamoja na Mwenyekiti wa Group Kilimanjaro Inc.